

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TANO

2 MEI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA TANO TAREHE 2 MEI, 2017

I. DUA:

Saa 3:00 Mhe. Job Yustino Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Nenelewa M. Wankanga
2. Ndugu Ramadhani Issa
3. Ndugu Joshua Chamwela

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

1. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangala aliwasilisha Mezani Randama za makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
2. Mhe. Almas Athumani Maige (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge aliwasilisha Mezani Taarifa zifuatazo:-
 - Taarifa kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalowahusu Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe na Mhe. Halima James Mdee;
 - Taarifa kuhusu shauri la kuingilia Uhuru na Haki za Bunge linalowahusu Ndg. Paul Christian Makonda na Ndg. Alexander Mnyeti;
 - Taarifa kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mhe. Ester Amos Bulaya.

III. MASWALI

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 119: Mhe. Peter Joseph Serukamba

Nyongeza: Mhe. Peter Joseph Serukamba
Mhe. George Malima Lubeleje

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 120: Mhe. Saumu Heri Sakala

Nyongeza: Mhe. Saumu Heri Sakala
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq
Mhe. Savelina Silvanus Mwijage

Swali Na. 121: Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula

Nyongeza: Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula
Mhe. Aida Joseph Khenan

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Swali Na. 122: Mhe. Amina Nassoro Makilagi (liliulizwa na Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia)

Nyongeza: Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia

Swali Na. 123: Mhe. Upendo Furaha Peneza

Nyongeza: Mhe. Upendo Furaha Peneza
Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 124: Mhe. Hussein Nassor Amor (liliulizwa na Mhe. Constantine John Kanyasu)

Nyongeza: Mhe. Constantine John Kanyasu

Swali Na. 125: Mhe. Oran Manase Njeza

Nyongeza: Mhe. Oran Manase Njeza
Mhe. Omar Yahaya Massare

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Swali Na. 126: Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel (liliulizwa na Mhe. Julius Kalanga Laizer)

Nyongeza: Mhe. Julius Kalanga Laizer
Mhe. Rhoda Edward Kunchela
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu

Swali Na. 127: Mhe. George Malima Lubeleja

Nyongeza: Mhe. George Malima Lubeleja

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Swali Na. 128: Mhe. Stella Alex Ikupa

Nyongeza: Mhe. Stella Alex Ikupa

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 129: Mhe. Ester Amos Bulaya

Nyongeza: Mhe. Ester Amos Bulaya
Mhe. Boniface Mwita Getere
Mhe. Frank George Mwakajoka

MATANGAZO:

1. Wageni wote walikaribishwa Bungeni.
2. Matokeo ya mechi kati ya Bunge na Morogoro Kombaini yalitangazwa
3. Zoezi la kubadilisha kadi za chanjo ya manjano litaanza leo.
4. Wafanyakazi bora wa Ofisi ya Bunge walitambulishwa.

IV. MIONGOZO

1. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya aliomba mwongozo kwa Kanuni 68(7) na 69(1) na kuomba Bunge liahirishwe ili kujadili jambo la dharura linalohusiana na athari za operesheni ya maliasili inayoendeshwa Jimboni Kaliua na kusababisha zaidi ya familia 100 kukosa makazi.
 - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) alisimama na kuomba Serikali ichukue jambo hilo, ifanyie kazi na kutoa Taarifa Bungeni baadae.
2. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare alitumia Kanuni ya 69(1) kuomba Bunge liahirishwe na kujadili tatizo la Tetemeko lililotokea Mkoani Kagera juzi na kuuliza mbona ripoti ya uchunguzi ya Kitengo cha Jiolojia kuhusu hali ya matetemeko Mkoani Kagera haijatolewa.

- Waziri wa Nishati na Madini alitoa taarifa kuwa Ripoti za Matetemeko zipo, zitatolewa na pia Mbunge atapewa nakala.
3. Mhe. Julius Kalanga Laizer aliomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 46 kuwa majibu ya Swali lake la Nyongeza kwa Swali namba 126 hayakuwa ya kuridhisha, halikujibiwa.
- Spika alimshauri Mbunge aonane na Waziri husika ili apate maelezo zaidi ya swali lake.

V. HOJA ZA SERIKALI

- Mhe. Almas Athumani Maige, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge alisoma Taarifa na Maazimio ya Kamati kuhusu hoja zifuatazo:-
 - (i) Shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalowahusu Mhe. Freeman Aikael Mbowe na Mhe. Halima James Mdee;
 - (ii) Shauri la kuingilia Uhuru wa Haki za Bunge linalowahusu Ndg. Paul Makonda na Ndg. Aleander Mnyeti;
 - (iii) Shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

Wachangiaji wa Hoja ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

- | | | |
|--------------------------------------|---|------------|
| 1. Mhe. Joseph Roman Selasini | - | CHADEMA |
| 2. Mhe. Riziki Shahari Mngwali | - | CUF |
| 3. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola | - | CCM |
| 4. Mhe. Peter Joseph Serukamba | - | CCM |
| 5. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia | - | CCM |
| 6. Mhe. Abdallah Majura Bulembo | - | CCM |
| 7. Mhe. Jannet Zebedayo Mbene | - | CCM |
| 8. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | - | CCM |
| 9. Mhe. George Boniface Simbachawene | - | CCM |
| 10. Mhe. Jenista Joakim Mhagama | - | Chief Whip |

Mhe. Jenista Joakim Mhagama, kwa kutumia Kanuni 57(1) alitoa Hoja ya kubadilisha maneno yaliyotumika kwenye Azimio linalomhusu Halima Mdee yabadilishwe kwa kuongeza maneno "Ninaomba Bunge liazimie kwamba Mhe. Mdee asamehewe kwa kosa alilofanya, ila tu ikiwa atafanya kosa jingine utekelezaji wa adhabu uanze akifanya kosa kama hili tena hata kulazimika kupelekwa kwenye Kamati."

Spika aliwahoji Wabunge kuhusu Hoja ya mabadiliko iliyowasilishwa na Mhe. Jenista Mhagama na Bunge lilikubali mabadiliko hayo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati (Mtoa Hoja) alihitimisha Hoja zote tatu. Kisha Spika aliwahoji Wabunge kuhusu Maazimio yote matatu pamoja na marekebisho yaliyofanyika kwenye Azimio la Mhe. Halima James Mdee. Aidha Mhe. Halima Mdee amepewa sharti kwamba akifanya kosa jingine ataadhibiwa bila ya kulazimika kupelekwa kwenye Kamati ya Maadili, na pia Mhe. Ester Bulaya atalazimika kupewa barua ya onyo.

Baada ya uamuzi huo Spika alitoa maneno ya jumla ya Rai kwa Wabunge/Watumishi kuzingatia Maadili/Kanuni na kutoichafua Taasisi ya Bunge. Aidha, aliwasamehe wote wanaofanya vitendo hivyo.

VI. KUSITISHA BUNGE

Saa 7 mchana Spika alisitisha Bunge hadi saa 11:00 Jioni.

VII. BUNGE KUREJEA

Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia na kuongozwa na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mwenyekiti).

VIII. HOJA ZA SERIKALI

Uchaguzi wa Hoja ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano uliendelea kwa Wabunge wafuatao kuchangia:-

- | | | | |
|-----|------------------------------|---|-----|
| 58. | Mhe. Bonnah Moses Kaluwa | - | CCM |
| 59. | Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia | - | CCM |

60.	Mhe. Joseph Michael Mkundi	-	CHADEMA
61.	Mhe. Selamani Said Bungara	-	CUF
62.	Mhe. Hamidu Hassan Bobali	-	CUF
63.	Mhe. Fredy Atupele Mwakibete	-	CCM
64.	Mhe. Josephat Simkamba Kandege-	-	CCM
65.	Mhe. Julius Kalanga Laizer	-	CHADEMA
66.	Mhe. Yahaya Omary Massare	-	CCM
67.	Mhe. Selamni Said Jafo	-	Naibu Waziri
68.	Mhe. Edwin Amandus Ngonyani	-	Naibu Waziri

IX. KUHITIMISHA HOJA

Mtoa Hoja, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano alihitimisha Hoja yake kwa kujibu Hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge na kisha kutoa Hoja ambayo iliungwa mkono kisha Bunge likaingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi.

FUNGU 68- MAWASILIANO

Lilichangiwa na Wabunge Wafuatao:-

1. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya
2. Mhe. Ahmed Juma Ngwali – alitoa shilingi na kisha kuirudisha
3. Mhe. Stephen Hilay Ngonyani – alitoa shilingi na kuirudisha baada ya uamuzi wa kupeleka Hoja yake kwenye Kamati ya Bajeti.
4. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa
5. Mhe. Desderius John Mipata
6. Mhe. Silafu Jumbe Maufi
7. Mhe. Japhet Hasanga

Kufuatia kwisha kwa muda, Bunge lilingia kwenye hatua ya *guillotine* na kupitisha fungu hilo la 68, 98 na 62 bila mabadiliko yoyote.

Mtoa hoja alitoa Taaria ya kazi ya kamati, Bunge lilihojiwa na kupitisha Bajeti ya Wizara hii.

X. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 2:10 usiku Mwenyekiti aliahirisha Bunge hadi tarehe 3 Mei, 2017 saa 3:00 asubuhi.